Nuru ya Kiswahili, Juzuu 5(1), Juni 2026:68-92
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru51.6892

# Changamoto za Uandishi wa Miswada ya Filamu za Kiswahili Nchini Tanzania

**Gervas A. Kasiga**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dodoma**
kassiga@gmail.com

## Ikisiri

Makala hii inajadili changamoto za uandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Msukumo wa utafiti wa makala ulichangizwa na maoni ya hadhira ambayo yalibainisha kutofuatiliwa kwa filamu za Kiswahili hutokana na udhaifu wa ujenzi na uwasilishwaji wa hadithi. Utafiti umetumia mikabala ya kihistoria, kiteknolojia, kibiashara na kimasoko kama kiunzi cha ukusanyaji, uchambuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo. Mbinu za kitaamuli ndizo zimeendesha hatua zote za kitafiti. Makala inawasilisha changamoto mbalimbali zinazorudisha nyuma ubora wa miswada na filamu zinazotayarishwa. Nazo ni: ukosefu wa elimu na mafunzo ya uandishi wa miswada ya filamu kwa waandishi, ufinyu wa bajeti za kutayarishia filamu, kutofanyika kwa tafiti kabla ya uandishi wa miswada, pamoja na upungufu wa ubunifu wa uandishi wa miswada. Nyingine ni: mabadiliko ya mifumo ya mawasiliano ya kiteknolojia, ukosefu wa uhuru wa ubunifu, pamoja na udhaifu wa soko na hakimiliki. Ili kuboresha uandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili nchini Tanzania, yafuatayo yanapendekezwa na makala hii: kutengenezwa kwa mitaala maalumu ya mafunzo kwa waandishi wa miswada ya filamu ili kuboresha uwezo wao, kutayarishwa kwa programu atamizi kwa waandishi wa miswada, idara zinazohusika na lugha na fasihi ya Kiswahili ziboreshe mitaala kwa kuihusisha fasihi na filamu, kuwapo kwa mashindano ya uandishi wa filamu za Kiswahili, pamoja na kurahisisha upatikanaji wa nyaraka za kitafiti ili kuboresha maandishi ya miswada kwa waandishi.

**Dhana za Msingi:** filamu, hadithi, mswada wa filamu

## Utangulizi

Tangu fani ya filamu ilipoasisiwa na Lumière brothers mwaka 1895 kupitia filamu ya "*Workers Leaving the Lumière Factory*" (Abel, 1994), imeendelea kuwa chombo muhimu cha kuwasilisha mawazo ya kijamii na kuburudisha. Wataalamu wengi wameichambua na kuihakiki filamu kwa muktadha wa teknolojia ya utayarishaji (Giannetti, 1986). Hata hivyo, kuna wataalamu wengine wameihusisha filamu kwa mtazamo wa sanaa za kuonwa na sanaa za maonesho (Gumbo, 2019; Majembe, 2023). Wamehusisha namna filamu inavyotoa fursa za kiajira, masoko yake pamoja uharamia katika kazi zake (Kabyemela, 2017). Hata hivyo, katika miaka ya karibuni, baadhi ya watafiti wameona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuinasibisha filamu na fasihi (Mrikaria, 2007; Abdallah, 2018). Wameitafsiri filamu kama fasihi simulizi iliyopevuka (Kasiga, 2013; Kasiga na Luhwago, 2020). Zaidi ya hivyo, filamu imetazamwa kama sanaa inayoundwa kwa modeli anuai. Katika hili, filamu imepambanuliwa kwa jinsi inavyotumia lugha za namna mbili katika kusema hadithi yake. Mosi ni lugha ya kawaida ya kimaongezi inayotendwa na waigizaji runingani pamoja na maandishi ya ufafanuzi yanayopita runingani kuelezea simulizi. Pili, ni lugha inayoletwa na uchukuaji wa picha jongevu zenye kutengeneza namna fulani ya kipekee ya mawasiliano ya maudhui kutoka kwa mwongozaji wa filamu kwenda kwa hadhira (Mahenge, 2016).

Mitazamo mipya yote imeitazama filamu kifasihi kutoka kwenye dhana ya hadithi ambayo ndiyo kiini cha simulizi ya filamu (Shukla, 2013; Kasiga, 2013). Kimsingi, mitazamo hiyo inatoa tafsiri kwamba vifaa vya kiteknolojia haviwezi kumsaidia mwongozaji wa filamu kutamba hadithi yake ya kifilamu bila kuwako kwa mambo makuu matatu ya msingi. Jambo la kwanza ni simulizi ambayo hubeba dhana ya hadithi. Jambo la pili ni

dhana ya umithilishaji, ambapo maisha ya wanadamu huakisiwa kisanaa kupitia filamu. Jambo la tatu ni mwandishi wa mswada ambaye ndiye huchora dira ya filamu kimaandishi kwa kutumia lugha fulani inayozungumzwa na jamii inayolengwa na kazi husika. Hii inadhihirisha kuwa ni vyema kuitazama filamu—hadithi inayosimuliwa—kwa mtazamo wa lugha na fasihi yake ili kusaidia ukuaji wake kupitia mzizi wake mkuu. Kufanya hivyo huongeza tija za ukuaji wa filamu kwa miktadha yote ya ukuaji wa mawasiliano kupitia lugha na uchukuaji wa picha jongevu zenye kuleta athari iliyokusudiwa kwa watazamaji. Vilevile, kutaendelea kudhihirisha ukuaji wa fasihi kupitia maendeleo ya teknolojia kuanzia mdomo, maandishi na sasa utambaji jongevu kupitia njia za kidijiti.

Mdhihiriko wa filamu huanzia kwenye mswada wa filamu. Hili ni andiko maalumu la kibunifu linaloandikwa ili kuwa mwongozo wa utayarishaji wa filamu, tamthiliya ya runinga au kazi yoyote ya kibunifu inayolengwa kwenda kusimulia jambo fulani kupitia picha jongevu (Howard na Mabley, 1993). Mswada wa Filamu huzalishwa kutoka kwenye wazo la kibunifu la mwandishi wa mswada. Mswada hujengwa na mambo muhimu kama vile maelezo ya msingi kuhusu wahusika, maelezo ya vitendo vinavyofanywa na wahusika, dayalojia za kuzungumzwa na waigizaji, maelekezo muhimu ya hisia za kutekelezwa na waigizaji, na maelekezo ya mahali na wakati wa tukio la simulizi ya filamu. Mambo yote hayo huhitaji ubunifu wa kiwango cha juu katika kuyaandika ili yaweze kuleta mswada bora wa kutayarisha filamu ya viwango vya kimataifa.

Kimsingi, filamu haiwezi kupata ukamilifu wake bila kuwapo kwa mswada bora wa filamu. Hata hivyo, machapisho ya kitaaluma, maoni mengi ya hadhira kutoka mitandaoni, pamoja na takwimu zinazoeleza kutokupanda

kwa mauzo ya filamu za Kitanzania hujielekeza kwenye muundo na uwasilishaji wa hadithi ya filamu (Gumbo, 2019; Kasiga, 2024). Hadhira ya filamu imekuwa ikieleza kuwa kukosekana kwa mvuto wa masimulizi ya hadithi ya filamu kama sababu ya kutotazamwa kwa filamu za Kitanzania. Kutokana na ubora wa hadithi ya filamu kujengwa na miswada yake, tuliona ni muhimu kufanya utafiti uliozalisha makala hii. Shabaha kuu ilikuwa kubaini changamoto za uandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili. Pia, tulikusudia kutoa mapendekezo yatakayosaidia kukabiliana, kupunguza au/na kuondoa changamoto zilizobainika kushusha kiwango cha uandishi wa miswada ya filamu nchini Tanzania.

## Methodolojia ya Utafiti

Utafiti ulifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ya nchini Tanzania kwa sababu zifuatazo: Mosi, mikoa hiyo miwili ni eneo kuu la utayarishaji wa filamu na biashara yake. Pili, ni mikoa yenye shughuli za kiserikali za ujengaji wa sera za ukuzaji na uendelezaji wa filamu nchini Tanzania. Utafiti ulitumia majadiliano ya vikundi lengwa kupitia mtandao wa kijamii wa *facebook*, ambapo ilifanyika mijadala mitano ya vikundi lengwa viwili kutoka kwa waandishi wa miswada. Aidha, utafiti ulihoji watafitiwa hamsini. Halikadhalika, ulipitia miswada minane ambayo nayo filamu zake zilitafitiwa. Sampuli hiyo ilipatikana kutokana mbinu za usampulishaji lengwa. Utafiti ulifanyika uwandani ili kupata taarifa za msingi kutoka kwa wahojiwa. Pia, ulifanyika maktabani ili kupata taarifa za ziada kutoka miswada ya filamu na uchanganuzi wa kina wa filamu.

## Changamoto za Uandishi wa Miswada ya Filamu za Kiswahili

Sehemu hii inawasilisha changamoto za uandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Hoja zinazowasilishwa na kujadiliwa ni:

ukosefu wa elimu na mafunzo ya kitaalamu ya uandishi wa miswada ya filamu, ukosefu wa utafiti wa kina katika mada zinazoandikiwa miswada ya filamu, na upungufu wa ubunifu wa uandishi kwa miswada inayoandikwa. Nyingine ni: ufinyu wa bajeti na masoko, kubinywa kwa uhuru wa mwandishi katika kujenga mawazo bunifu ya kihadithi, masuala yanayohusiana na hakimiliki ya miswada, pamoja na mabadiliko ya teknolojia ya kisasa ya mawasiliano.

**Ukosefu wa maarifa rasmi ya uandishi wa miswada**

Maarifa hupatikana kupitia elimu rasmi au mafunzo ya kitaalamu yatokewayo kwa muda mfupi. Ilibainika kuwa waandishi wengi wanaoandika miswada ya filamu wamebainika kutokuwa na elimu rasmi ya kifilamu, hususani katika eneo la uandishi wa miswada. Jambo hilo limesababisha kukosa mbinu sahihi za kuandika miswada itakayoleta athari inayokusudiwa kwa hadhira ya filamu za Kitanzania. Watayarishaji wengi hujifunza uandishi wa filamu kupitia utazamaji wa filamu pamoja na kipaji. Hivyo, wanakosa mbinu kuntu za kufanya miswada yao ya filamu iwe bora. Katika kulifafanua hili, Mtafitiwa wa Kwanza[1] anaeleza:

> Kuna uhaba wa waandishi waliopitia mafunzo rasmi ya uandishi wa Filamu. Waandishi wengi hawana elimu rasmi ya *screenwriting* (uandishi wa miswada ya filamu). Wengi wao huandika kutokana na uzoefu wa kawaida bila kufuata kanuni za kitaalamu za uandishi wa miswada. Kujifunza kwao misingi ya uandishi wa filamu kumejikita katika kuangalia filamu na kuiga bila kuelewa nguzo kama vile; namna ya muundo wa hadithi wa hadithi ya filamu, kujenga na kuendeleza tabia za wahusika, uundaji wa migogoro endelevu ya kihadithi pamoja na midundo na kani ya

[1] Huyu ni Afisa Maendeleo ya Filamu kutoka Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini Tanzania. Mahojiano haya yamefanyika tarehe 14 Mei 2025 - Kivukoni, Dar es Salaam.

> kisimulizi (Ufafanuzi wa kwenye mabano ni wa mwandishi wa makala).

Maoni ya mtafitiwa yanadhihirisha kwamba ukosefu wa taaluma ya uandishi miswada ni sababu kubwa inayofanya filamu zinazozalishwa kukosa muundo bora na mvuto wa kiutazamaji, licha ya kuwa mawazo mazuri ya kihadithi. Kwa hali hiyo, asilimia kubwa ya waandishi hujikuta wakiandika miswada isiyokamilika. Hii inasababisha filamu zinazotayarishwa kutegemea mwongozo wa vipande vya mchezo vyenye maelekezo ya kutendwa na wahusika vitumike kutayarishia filamu. Hali hiyo huwafanya waigizaji kuigiza kwa namna faraguzi kwa kukosa matukio yenye ruwaza bora pamoja na kuwa na mazungumzo yasiyo na mantiki.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa waandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili nchini Tanzania wamekosa mafunzo ya kitaalamu ya uandishi wa filamu katika eneo la uandishi wa filamu. Mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa kupitia warsha na semina mbalimbali za filamu. Hali hii imeendelea kuchochea uzalishwaji wa miswada inayokosa mvuto au upekee kutokana na kuwa na muundo dhaifu. Kimsingi, uandishi ni fani inayohitaji kuzamiwa ili kuweza kutengeneza na kuwasilisha falsafa zinazotambulisha utu, utaifa na utamaduni wa jamii. Katika kulikazia suala hili Mtafitiwa wa Pili[2] anaeleza:

> Ninasisitiza kuwa uandishi wa mswada wa filamu ni taaluma na uandishi wa hadithi ni kipaji. Mtu yoyote mwenye uwezo wa kuelezea au kuandika hadithi anaweza kufanya hivyo na kipaji chake kikaonekana. Ila, siyo kweli au rahisi kwa mwandishi wa mswada wa filamu asiyekuwa na taaluma hiyo akaandika na kutengeneza filamu

[2] Huyu ni mwandishi wa miswada ya filamu na riwaya maarufu. Hivi sasa, ameshatangulia mbele ya haki. Mahojiano haya yalifanyika kupitia mtandao wa kijamii wa *facebook* Oktoba 21, 2018.

> ikaeleweka kwa maana ya filamu hasa, achilia mbali uzuri au ubaya wa filamu hiyo. Kama unafanya utafiti wa kupata waandishi wa miswada ya filamu waliosomea hasa hapa nchini kwetu, basi unaweza ukawahesabu kwa vyanda vyako vya mikono. Lakini ukitaka kutuhesabu sisi akina 'Ngoma iko' hata ukitumia nywele zako zitakwisha lakini hutatumaliza…

Mtafitiwa alikuwa anakazia namna elimu ya uandishi wa miswada ya filamu ilivyo muhimu katika utayarishaji wa filamu bora. Ameonesha bayana kuwapo kwa idadi kubwa ya waandishi waliokosa maarifa ya uandishi wa filamu ambayo yangeweza kunyanyua ubora wa tasnia nzima ya filamu. Jambo hili linakaziwa na Mtafitiwa wa Tatu[3] kwa kusema:

> Uandishi wa miswada ni taaluma. Ni zaidi ya kipaji. Kuna vitu vingi sana vya kuzingatia ambavyo kama huvijui huwezi kuandika cha kueleweka kifilamu. Kwa mfano, uandishi wa dayalojia za kifilamu, ujenzi wa taharuki, uundaji wa wahusika pamoja na utengenezaji wa mantiki za matukio kwa hadhira si vitu vya kuamka na kufanya tu! Kimsingi, si kila hadithi yaweza kuwa filamu. Vinginevyo apatikane mbobevu wa kuifanya iwe mswada. Hapo ndipo tunakosa wataalamu wa namna hiyo wanaotokana na ujuzi wa darasani…

Kwa kuzingatia maoni ya watafitiwa, ilibainika kwamba kutokufuata vigezo vya kitaaluma vya kiuandishi kumesababisha kuzaliwa kwa miswada mingi dhaifu. Kwa hali hiyo, filamu nyingi zinazotayarishwa zimekuwa zikikosa vigezo vya kimataifa kuendana na soko la ushindani la kimataifa. Jambo hilo limekuwa likisababisha kudidimia kwa kipato wanachokipata wanatasnia wa filamu na michezo ya kuigiza nchini Tanzania.

[3] Huyu ni mwandishi wa miswada ya filamu na mtangazaji wa Kituo cha Utangazaji cha Kimataifa. Mahojiano haya yalifanyika kwa njia ya mtandao wa kijamii wa *facebook* Februari 06, 2024.

**Ufinyu wa bajeti za kutayarishia filamu za Kiswahili**

Ufinyu wa bajeti zinazopangwa kwa ajili ya utayarishaji wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania nao umebainika kuwa chanzo cha kudorora kwa ubora wa miswada ya filamu. Kutokana na ufinyu wa bajeti za utayarishaji wa filamu, waandishi wa miswada wamekuwa wakilipwa ujira mdogo kwa kazi yao. Aghalabu, ujira ambao waandishi wa miswada wamekuwa wakilipwa katika uandishi wa miswada ya filamu na tamthiliya za runinga huwa ni kati ya shilingi za Tanzania 200,000 hadi 800,000. Kimsingi, hiyo ni bajeti ndogo ya kuweza kumfanya mwandishi aweze kuandika mswada utakaokuwa na tija kwake na katika soko. Hili limekuwa likisababisha waandishi wa miswada ya filamu kuandika miswada kwa haraka bila ya utulivu ili waweze kuishi. Mathalani, kwa bajeti hiyo, mwandishi wa miswada hujikuta akiandika miswada ya watu wawili au zaidi kwa wakati mmoja ili aweze kupata kipato cha kukidhi mahitaji yake. Nguvu kubwa ya uandishi hujikuta iko katika kukusanya fedha na si kuhakikisha anaandika mswada bora wa kutengenezea filamu. Hoja hii inapambanuliwa na Mtafitiwa wa Nne[4] ambaye anasema:

> Waandishi wengi hulazimishwa kukamilisha miswada ndani ya muda mfupi. Hali hiyo hupunguza ubora na ubunifu kwa mwandishi na kusababisha mswada unaoandikwa kuwa na mapungufu katika mwendelezo wa hadithi na wahusika. Jambo hilo hufikia wakati linagunduliwa na watazamaji wengi na kuzikosoa kwa haraka na wepesi. Kwa mfano, katika moja ya filamu ambayo nilishiriki kuandaa, nilishangazwa kuona mwandishi wa mswada amepewa wiki moja kuandaa mswada wa tamthiliya ya runingani. Kinyume na matarajio, aliandika. Hata hivyo, tamthiliya ilipokamilika na

[4] Huyu ni Afisa Maendeleo wa Filamu kutoka Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania anayeshughulika na uhakiki wa miswada ya filamu na tamthiliya inayopitiwa na Bodi hiyo. Mahojiano haya yalifanyika Disemba 06, 2024, Kivukoni, Dar es Salaam.

> kurushwa, ilikosolewa na watazamaji pindi tu imeanza kuonyeshwa kwenye runinga…

Kimsingi, mtafitiwa anafafanua kuwa hali ya ufinyu wa bajeti ni kikwazo kinachoathiri mchakato mzima wa utayarishaji wa filamu. Jambo hili limebainika kuanzia katika uandishi wa mswada husika. Kihalisi, uandishi wa mswada wa filamu au tamthiliya ya runinga ni mchakato unaohusisha uandikwaji wa rasimu nyingi hadi kufikia rasimu ya mwisho inayotumika kutayarishia filamu. Rasimu hizo huchukua maoni mbalimbali ya kiuboreshaji kutoka kwa wabobevu wa uandishi na wahariri wa miswada ili kupata mswada bora. Utafiti uliozalisha makala hii ulibaini kuwa, aghalabu, uandishi wa mswada wa filamu nchini Tanzania hufanywa na mtu mmoja pekee. Kutokana na jambo hilo, mwandishi hukosa nafasi ya kujikosoa na kufanya marekebisho ya kina. Mtafitiwa wa Nne anathibitisha hili kwa kurejelea namna ilivyofanyika katika tamthiliya ya runinga aliyoshiriki. Anaeleza:

> Kwa mfano, wakati wa utayarishaji wa tamthiliya niliyoshiriki[5], timu ya utayarishaji ilikiri kuwa mswada uliandikwa rasimu moja tu kabla ya kuanza kurekodiwa. Vilevile, hata rasimu hiyo moja haikupata wasaa wa kupitiwa na timu nzima ya utayarishaji, zaidi ya kupewa waigizaji kuanza kuifanyia kazi kwa siku moja ili iweze kurekodiwa. Sasa, matokeo yake, baadhi ya matukio yaliyorekodiwa yalibainika kutokuwa na uhalisi. Pia, motifu za matukio kwa wahusika hazikueleweka vizuri. Hata hivyo, hakukuwa na njia nyingine. Tamthiliya hiyo ilikuwa tayari ikioneshwa runingani…

Jambo hili linabainisha wazi kuwa yote haya hufanyika kwa haraka ili kuweza kuendana na bajeti iliyopo. Madhara yake yamekuwa makubwa

[5] Anaitaja tamthiliya hiyo. Hata hivyo, kwa sababu za kibiashara na hakimiliki hatuitaji tamthiliya hiyo katika makala hii.

kwa eneo la uandishi ambalo ni kiini cha utayarishaji wa filamu. Pia, yamekuwa na athari katika mfumo mzima wa utayarishaji wa filamu. Fauka ya hayo, ilibainika kuwa licha ya miswada kutopitiwa, bado miswada hiyo huwa haipewi thamani yake wakati wa utengenezaji wa filamu. Mathalani, miswada iliyoandikwa hubadilishwa inapofika katika mandhari ya utayarishaji na kukifanya kile kinachoandikwa kisiwe kile kinachorekodiwa. Hali hiyo hufanya uhalisi ukosekane kutokana na kubadilisha sura nzima ya filamu iliyotarajiwa kutengenezwa.

Halikadhalika, ilibainika kuwa kutokana na ufinyu wa kibajeti waandishi wengi wamekuwa wakitumia njia za kawaida za kuandikia miswada ya filamu, badala ya kutumia programu maalumu za uandishi wa miswada. Wengi wa waandishi wa miswada ya filamu wamekuwa wakitumia *Microsoft word* badala ya programu za uandishi miswada za *Celtx* na *Final Draft*. Hili limedhihirishwa na Mtafitiwa wa Nne ambaye anakiri kuwa miswada mingi ambayo wamekuwa wakiipokea ili kuihakiki imekuwa ikiandikwa pasi na kutumia programu hizo. Zaidi, ilibainika kuwa miswada mingine wanayoipokea imekuwa ikiandikwa kwa mkono, tena katika madaftari ya kawaida, na kuwasilishwa ili kuweza kupatiwa vibali vya utayarishaji. Changamoto hii imekuwa ikiwakumba waandishi ambao hawana mafunzo rasmi pamoja na nyenzo nyingine muhimu za kiuandishi. Pia, waandishi wa namna hii wamekuwa wakikosa ujuzi wa kutumia kompyuta.

Hali hii imekuwa ikiwavunja moyo waandishi wa miswada na kushusha uwekezaji wa muda wao katika uandikaji wa miswada ya filamu yenye vigezo. Katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa filamu, bei ya kuuza kazi ya filamu huendana na uwekezaji uliowekwa kwenye mchakato mzima

wa utayarishaji wa filamu. Uwekezaji huo ndio huamua ubora wa ubunifu na maandalizi ya jumla ya utengenezaji wa filamu. Katika utayarishaji wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania uwekezaji finyu katika utayarishaji wa filamu unaathiri uandikwaji wa miswada ya filamu. Hali hiyo huathiri malipo bora kwa waandishi wa miswada. Hili limewafanya waandishi nao kutowekeza muda wao katika ubunifu, hivyo kusababisha kuzalishwa kwa kazi sizizokidhi viwango.

Hivyo basi, waandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili wamekuwa wakiandika filamu nyingi kwa wakati mmoja ili kupata kipato zaidi. Hilo nalo limezidi kufanya kazi zao kuwa na kiwango duni. Matokeo yake, tasnia ya filamu za Kiswahili nchini Tanzania imekuwa ikitoa filamu nyingi kwa kigezo cha idadi na si kwa kigezo cha ujumi wa filamu zinazotayarishwa (Kasiga, 2024). Waandishi wa miswada wamekuwa wakiandika filamu kwa kuweka mtazamo wa kupata pesa ya kuwaondolea matatizo yao ya mara moja na si kuandika filamu ambazo zinaweza kuishi na kuitangaza Tanzania kwa namna nyingi zenye kuvutia mataifa mengine. Hii ni kwa sababu, filamu zinazotayarishwa kutokana na miswada isiyokidhi vigezo imekuwa ikishindwa kubeba vyema dhana kuu ya filamu kwa mawasiliano. Zaidi, zinakosa dhamira madhubuti za mabadiliko chanya pamoja na madhumuni ya kazi ya sanaa kwa jamii, hivyo kudumaza maendeleo ya tasnia nzima kwa ujumla.

**Kutofanyika kwa utafiti kabla ya uandishi wa miswada**

Utafiti wa uliozalisha makala ulibaini kwamba kutofanyika kwa utafiti kabla ya uandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili kunadumaza ubora wa filamu zinazotayarishwa. Hii ni kwa kuwa, ili miswada ya filamu iwe bora ni muhimu kuhakikisha kunakuwa na utafiti na uchambuzi wa kina

unaogusa maisha halisi ya kijamii. Kwa kufanya hivyo, husaidia masuala yanayoandikwa kuaminika na jamii na, hivyo, kuyaona kuwa ni sehemu ya maisha yao. Pia, husogeza karibu dhana ya umithilishaji wa maisha ya kijamii katika kazi ya kisanaa. Hata hivyo, ilibainika kuwa miswada mingi inayoandikwa haipitii mchakato wa utafiti; hivyo husababisha maudhui yake kutobeba uhalisi. Miswada imekuwa ikiandikwa kwa kubeba dhana na mitazamo isiyo ya kina inayomgusa mwandishi pekee. Kwa mantiki hiyo, mwegamo wa simulizi, ujenzi wa wahusika, matendo yanayofanyika, matukio yanayofanyika, miktadha, pamoja na uakisi wa maisha huwa kinyume na dhana nyingi halisi za kijamii. Katika kukazia hoja hii, Mtafitiwa wa Nne anafafanua:

> Miswada mingi ya filamu huandikwa bila kufanyika kwa tafiti. Wasichofahamu ni kwamba, mswada mzuri na bora unahitaji utafiti wa kina kuhusu mada husika. Hiyo husaidia kuandika hadithi na wahusika wa kuaminika ili kuleta uhalisia. Lakini, hadithi nyingi za filamu za hapa nchini huandikwa kwa mitazamo ya juujuu ya mwandishi…

Maoni ya mtafitiwa yanabainisha namna miswada bora inavyotakiwa iwe. Yanadhihirisha kuwa kukosekana kwa tafiti za kina kabla ya kulifanya wazo la kihadithi la kifilamu kuwa filamu huondoa ubora wa filamu zinazotayarishwa.

Halikadhalika, hali ya waandishi wa miswada kutokufanya tafiti za kina kabla ya kuwasilisha mawazo yao katika muundo wa miswada huzifanya filamu nyingi kufanana; hivyo kusababisha kukosekana kwa upekee wa kibunifu. Zaidi, kama asemavyo Kasiga (2018), huchochea uigaji-pofu wa namna ya kuandika filamu kutoka mataifa mbalimbali (kama vile Naijeria,

Marekani, Korea Kusini na India). Hoja hii inatiliwa nguvu na Mtafitiwa wa Tano[6] kwa kusema:

> Unajua, katika jitihada za kupunguza gharama na kupata filamu zinazouzwa haraka, sisi waandishi hatuna budi kuiga filamu zilizowahi kufanikiwa. Tunakosa muda wa kubuni hadithi mpya. Ndiyo maana miswada yetu inafanana sana katika maudhui, wahusika na muktadha, jambo linalopunguza ubora na utofauti katika tasnia yetu…

Nukuu hii inatudokezea suala la kuwa na bajeti finyu linaonekana kuibua changamoto ya kutofanyika kwa utafiti wa kina kabla ya uandishi wa miswada. Kutokana na hali hii, waandishi hujikuta wakishindwa kufanya tathmini ya kina kuhusu jambo wanalohitaji kuliwasilisha. Ilibainika kuwa, wakati mwingine, waandishi wa miswada huwa na mawazo mazuri lakini kutokana na kutofanya utafiti, hushindwa kuyawasilisha kwa namna iliyo bora zaidi.

**Upungufu wa ubunifu wa uandishi wa miswada**

Ilibainika kuwa waandishi wengi wa miswada hukosa ubunifu, hivyo huandika miswada chini ya matarajio ya hadhira. Mathalani, katika miswada inayoandikwa kumekuwa na mawazo ya kihadithi yanayojirudia. Miswada mingi hubeba maudhui yenye mwegamo wa mapenzi. Licha ya miswada hiyo kusheheni dhamira za mapenzi, bado ndani yake kulidhihirika kukosekana kwa falsafa ambayo imejikita kuzungumzia uhusiano wa kimapenzi kwa mawanda mapana. Waandishi wengi wa miswada wamekuwa wakiamini kuwa hadhira inavutiwa na masuala ya kimapenzi. Hivyo, wamekuwa wakishindwa kuwa wabunifu kwa kugusa masuala mbalimbali ya kijamii ambayo yangeweza kuleta tija katika

[6] Huyu ni mwandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili na mpigapicha maarufu jijini Dar es Salaam. Mahojiano haya yalifanyika Kigamboni, Machi 17, 2025.

mabadiliko ya kitabia kwa jamii. Hali hiyo imezifanya filamu zinazotayarishwa kukosa nguvu kubwa ya kiushawishi ya kimawasiliano kwa hadhira.

Waandishi wameshindwa kubuni na kujaribu mwelekeo mpya wa hadithi ambazo zingeweza kugusa hisia za watazamaji. Hapa tunakusudia hadithi zenye miegamo kama vile ya kisayansi na teknolojia, kumbukumbu za matukio adhimu ya kitaifa, wasifu wa viongozi wakubwa wa kitaifa na kimataifa, tunu mbalimbali za utamaduni, pamoja na kukwamua mpotoko wa maadili ya jamii. Katika kuweka uzito wa hoja hii, Mtafitiwa wa Sita[7] anaeleza:

> Kumekuwa na malalamiko ya waandishi wengi wa miswada ya filamu za 'kibongo' (Kitanzania) kuandika dhima za mapenzi na matatizo ya kifamilia zaidi kuliko matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisera. Jambo hili pia linastahili kujadiliwa. Naamini linachangiwa na rika la vijana kushikilia hatamu za tasnia ya filamu. Ukirudi kwenye *Stages za Maslow za Needs* (Hatua za Mahitaji ya Maslow), kupenda na kupendwa kuko katika hatua za mwanzo za mahitaji ya mwanadamu. Hivyo, umri wa vijana hawa ndio haswa unajibu swali la kwa nini miswada mingi ni ya kimapenzi. Mbaya zaidi, hakuna jambo ambalo kisaikolojia linalengwa kuathiri mawazo ya mtazamaji kiubora kutoka katika madhara kwenda kwenye tija... (Ufafanuzi wa kwenye mabano ni ya mwandishi wa makala).

Mtafitiwa anabainisha kuwa waandishi wengi wa miswada ya filamu nchini wana umri mdogo. Wengi wao ni vijana. Hivyo, mawazo makubwa yanayowaongoza katika uandishi wao yamekuwa yakigusa zaidi hisia za mapenzi. Hata hivyo, hilo halikubainika kuwa ni jambo baya. Changamoto

[7] Huyu ni mwandishi wa filamu mwenye Shahada ya Awali katika masomo ya Filamu na Fasihi. Vilevile, ni mchambuzi wa masuala ya sanaa mitandaoni. Mahojiano haya yalifanyika Januari 20, 2024 Kisasa, jijini Dodoma.

kubwa iliyobainika ni kukosekana kwa mambo kuntu yanayowasilishwa kutoka katika mapenzi. Kimsingi, mapenzi yanayozungumzwa yamekuwa yakishindwa kuwasilisha dhana za msingi za kisaikolojia au falsafa fulani zinazoweza kuleta tija katika maisha ya Watanzania.

Upungufu huu wa ubunifu umefanya waandishi kutotilia mkazo misingi ya kitaalamu ya uandishi wa miswada. Miswada iliyotafitiwa wakati wa utafiti uliozaa makala hii ilidhihirisha kuwapo kwa dayalojia nyingi kuliko vitendo vinavyovutia utazamaji wa hadhira ya kifilamu. Dayalojia hizo, kama asemavyo McKee (1997), huwa na dosari za kukosekana kwa sifa kama vile mantiki iliyojikita katika ruwaza ya kutoa taarifa muhimu za wahusika, kupeleka mbele simulizi ya hadithi ya filamu, pamoja na kutoa taarifa muhimu ya hadithi. Kitaalamu, dayalojia zenye sifa hizo ndizo zenye kuchochea umakini wa mtazamaji wa filamu katika kufuatilia hadithi na matendo yanayotendwa na waigizaji runingani. Akikazia fikra hii, Mtafitiwa wa Sita anasema:

> Ninabainisha changamoto hizi kama mwandishi niliyepata mafunzo ya uandishi wa miswada ya filamu. Ubunifu unapungua kupitia vipengele vingi. Kimojawapo ni uchaguzi wa maneno ya kutumia ili kufikisha ujumbe. Hii ni changamoto kwa waandishi wengi wanaofahamu misingi ya uandishi lakini wasiokuwa wabunifu. Ndiyo maana ile *'principle'* (kanuni) ya *'less is more'* (umuhimu wa kuandika maneno machache yenye mantiki kuntu) inatushinda waandishi wengi. Humo utakutana na kurudiarudia maneno yenye maana moja kwa kwa mara nyingi bila ulazima wowote wa kufanya hivyo… (ufafanuzi wa kwenye mabano ni wa mwandishi wa makala).

Hapa, mtafitiwa amefafanua jinsi ambavyo waandishi hawatilii mkazo suala la ubunifu katika kuandika miswada. Hili limeonekana kuchukuana na suala

la kutokuwa na maarifa sahihi ya uandishi wa miswada ya filamu kwa waandishi. Hata hivyo, imebainika kuwa hata waandishi wachache walio na maarifa nao wamekuwa wakizembea katika suala la ubunifu ili waandike miswada ya filamu kwa haraka ili kujipatia kipato kwa mapema. Kimsingi, hali hii ya uharaka wa kuandika miswada imekuwa ikichochea ufinyu wa ubunifu wa mawazo ya hadithi za kuandikia filamu. Waandishi wamekuwa hawajipi muda wa kuifahamu vizuri jamii wanayoiandikia filamu. Ieleweke kwamba filamu ni uwasilishaji wa utamaduni, uhalisi wa maisha kwa njia zote mbili, kuburudisha na kuelimisha. Hivyo, ili mwandishi awe bora huhitajika kuwa na ukwasi wa maarifa ya kimaisha. Hali ya waandishi wa miswada kutokuwa na muda wa kumakinikia mambo hayo husababisha wawe na ukata wa ubunifu.

**Kubadilika kwa teknolojia**

Ilibainika pia kuwa ukuaji wa teknolojia na mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia ya mifumo ya mawasiliano yameibua changamoto katika eneo la miswada ya filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Suala hili linachagizwa na ukuaji wa vifaa kama vile vifaa vya kurekodia filamu, programu za kuhariri filamu, pamoja na majukwaa mapya ya uwasilishaji wa filamu kwa hadhira. Hivi sasa, kupitia mabadiliko ya teknolojia, uzalishaji wa filamu umechukua njia mpya (Mrikaria, 2007), ambapo, filamu zimekuwa zikichukukua jukwaa jipya kupitia mitandao ya kijamii kama vile *YouTube, facebook*, *Instagram*, *Vimeo*, *TikTok*, na *Netflix* (Kasiga, 2022).

Kutokana na hali hiyo, waigizaji wamekuwa wakitayarisha filamu zao bila kuandika miswada, kuiandika kwa haraka bila tuo au/na wakati mwingine kutokuiandika kabisa. Watayarishaji wengi wa maudhui ya mtandaoni hutumia simu pekee kutayarisha maudhui yao. Hali hiyo huchangia kazi

wanazozitayarisha kupwaya katika vipengele vya maadili, falsafa na utamaduni wa Kitanzania. Zaidi, husababisha tamthiliya za mitandaoni zinazotayarishwa kukosa vigezo vya kimataifa vya utayarishaji wa filamu. Akizungumzia kuhusu hali hio, Mtafitiwa wa Pili anasema:

> Waandishi wengi wanaandika miswada kwa haraka na bila kina wakiamini kuwa wataweza kuunda filamu yoyote kwa kutumia mbinu za uhariri na teknolojia badala ya misingi imara ya hadithi. Hali hii inasababisha kutokea kwa filamu zenye miswada dhaifu zisizo na mwendelezo mzuri wa hadithi wala maendeleo ya kina ya wahusika ambayo ndiyo yenye kuleta athari inayopaswa kwa watazamaji wake…

Maoni haya ni ithibati kuwa hali ya maendeleo ya mifumo ya mawasiliano ya kiteknolojia huwasukuma watayarishaji wa mitandaoni kufanya kazi kwa pupa. Wanafanya hivi ili kupata kipato cha haraka kutoka katika mitandao inayolipa kwa kutumia kazi zao. Hii husababisha filamu wanazozitayarisha huwa za viwango vya chini. Pia, husababisha filamu hizo kushindwa kupata watazamaji wengi kama ilivyotarajiwa. Filamu za kimtandao zinazopata watazamaji wengi nazo zimekuwa zikilalamikiwa na watazamaji kutokana na maudhui yanayobebwa na filamu hizo kukosa maadili. Watayarishaji wa kazi hizo wamekuwa wakikumbana na mamlaka inayosimamia kazi hizo kwa kuzifungia kazi husika pamoja na watayarishaji hao kushiriki katika shughuli za utayarishaji wa filamu.

Zaidi, jambo hili limesababisha waandishi wa filamu kuathiriwa na maudhui ya mtandaoni wanayoyaona kutoka nchi mbalimbali, hivyo hujikuta wakiendelea kuyaiga maudhui hayo na kuyatengenezea filamu za Kiswahili. Hali hiyo imesababisha miswada mingi ya filamu iwe ya burudani tu pasi na kuakisi mambo mengine ya msingi kutoka katika jamii ya Kitanzania. Mambo hayo yangeweza kuwasilishwa kwa dhima ya kuleta

mabadiliko yenye tija kwa jamii. Hili limesababisha filamu nyingi zinazotayarishwa kujikita katika burudani ya haraka na si kuzingatia uandishi wa hadithi zenye ujumbe mzito wa maadili. Miswada mingi inayoandikwa kwa kulenga mitandao hujaa vichekesho, majadiliano mepesi, pamoja na visa vingi visivyo na muumano wa kimantiki.

**Kukosekana kwa uhuru wa ubunifu**

Kupitia utafiti uliozaa makala hii, ilibainika kuwa waandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili wamekuwa wakikumbwa na changamoto ya kukosa uhuru wa kufanya ubunifu wao kwa mawanda mapana. Imedhihirika kuwa, mara nyingi, waandishi wamekuwa wakifuata miongozo na mawazo ya watayarishaji wa filamu ili waweze kuwa na fikra ya kuandika miswada yao. Watayarishaji wa filamu wamekuwa wakijikita zaidi katika kuangalia soko pamoja na kupunguza gharama za utayarishaji na si kuangalia kiwango cha ubunifu kinacholengwa na waandishi wa miswada kwenda kwa jamii yao. Mathalani, ilibainika kuwa waandishi wa miswada ya tamthiliya za runingani hupangiwa cha kuandika na mtayarishaji kiasi cha kuuweka shakani uhuru wa kuwasilisha mawazo yao kwa jamii pana. Zaidi, ilibainika kuwa miswada inayoandikwa ni lazima ilenge itikadi na, kwa upana, falsafa ya vyombo vinavyoenda kuonesha tamthiliya hizo. Katika kuzidi kuweka mkazo katika hoja hii, Mtafitiwa wa Saba[8] anasema:

> Unajua miswada yangu ya tamthiliya wakati mwingine ninapoiona inakuwa si kama yangu hivi. Mimi nilikuwa na mawazo tofauti kabisa na tamthiliya zangu mnazozijua (anazitaja). Lakini, sijaweza hata kidogo kuandika kwa namna yangu. Inanibidi niishi. Hivyo, ninachoandika ni kilekile tu kilichokubaliwa na mtayarishaji ambaye naye anategemea matakwa ya kituo cha runinga ili aweze kuuza

[8] Huyu ni mwandishi wa miswada aliyejikita katika uandishi wa tamthiliya za runingani. Mahojiano haya yalifanyika Aprili 17, 2023 Upanga, Dar es Salaam, Tanzania.

> kazi yake. Vilevile, sisi tuna familia hivyo binafsi naandika kwa namna nisiyoipenda sababu sina jinsi. Nitaishije?

Mtafitiwa alikuwa akidhihirisha namna uandishi wa miswada isiyo na ubora unavyochochewa na maelekezo ya watayarishaji wa vituo vya runinga. Vituo vya runinga vimekuwa vikitoa pesa ya kuandikwa miswada kwa malengo ya vituo hivyo. Hivyo, waandishi hujikuta wakiandika ndani ya malengo hayo, hivyo kukosa ubunifu.

Changamoto ya ukosefu wa uhuru wa kibunifu pia imebainika kwenda sambamba na ufinyu wa upatikanaji wa taarifa ambazo zingeweza kuongeza tija ya kiuandishi kwa waandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili nchini. Mara nyingi, nyaraka za namna hii ni ngumu kupatikana kutokana na usiri wake au/na kubeba dhima za ulinzi na usalama wa nchi. Mtafitiwa wa Kwanza anathibitisha hoja hii kwa kusema:

> Shida kubwa ipo katika uhuru wa mwandishi kueleza simulizi zake pamoja na wepesi wa upatikanaji wa taarifa stahiki hasa katika hatua ya utafiti. Hivi ni vikwazo mno. Yapo mambo ambayo hatupaswi kuyajua. Hivyo, kupata undani wake ni ngumu sana. Mengine kama mwandishi hupaswi kuyasema. Hivyo, tunalazimika kuandika yale tu ambayo yameridhiwa yaonekane. Kwa mfano, mimi, niliwahi kutembelea maktaba kuulizia kama naweza kupata nyaraka zozote zinazohusiana na lile tukio la "Uamsho". Nikashauriwa nifike Habari Maelezo. Huko nako nikaelekezwa niende Maktaba Kuu. Nilipofika hapo nikaambiwa kuwa taarifa hizo zipo chini ya Usalama wa Taifa, hivyo, niende kupata kibali au nyaraka nichukulie huko. Nikajiuliza, mimi kweli niende geti la usalama naulizia nyaraka za "Uamsho"? Niliishia hapo…

Mtafitiwa alikuwa akijaribu kuelezea hali halisi ya ugumu wa upatikanaji wa taarifa zinazoweza kuboresha simulizi za filamu za Kitanzania. Ili kuepukana na changamoto hii, kwa mawazo yake anapendekeza kuwa

simulizi za kitaifa zirudi kwa jamii na familia husika. Anaonesha kwamba kwa kufanya hivyo, waandishi watafaidika katika ubunifu wao, huku familia za wahusika nazo zikinufaika.

**Kutokuwapo kwa uhakika wa masoko na ulinzi wa miswada**

Tasnia ya filamu nchini Tanzania imebainika kukumbwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa masoko. Soko kubwa la filamu za Kitanzania linategemea vituo vya runinga. Vituo hivyo vimekuwa haviwezi kukidhi idadi kubwa ya filamu na tamthiliya zinazozalishwa nchini Tanzania. Hali hiyo imekuwa ikiathiri utayarishaji wa filamu. Kimsingi, waandishi wamekuwa wakiathirika kwa kulipwa ujira mdogo. Hivyo, hulazimika kuandika miswada katika hali za chini, kiasi cha kuathiri soko zima la filamu. Hivi sasa, nchini Tanzania, soko la filamu limekuwa likitegemea vituo vya runinga vinavyomilikiwa na kampuni za AZAM, DSTV na StarTimes pekee. Jambo hilo limekuwa likileta changamoto kubwa kwa waandishi na tasnia nzima ya utayarishaji wa filamu.

Ukosefu wa soko la uhakika huenda sambamba na kupwaya kwa ulinzi wa miswada ya waandishi. Waandishi wa miswada wamekuwa wakikumbana na changamoto ya kulinda kazi zao. Hofu ya waandishi kuibiwa kazi zao imewafanya waogope kushirikiana na wataalamu wengine wanaohariri miswada, waongozaji, na watayarishaji wa filamu. Waandishi wengi wamekuwa wakikosa hamasa ya kusajili kazi zao katika chombo cha usimamizi wa haki bunifu nchini (COSOTA). Kutokana na hilo, kumekuwa na migogoro mingi ya madai ya kazi za waandishi kutumiwa kutengeneza filamu na tamthiliya bila ridhaa ya waandishi wa miswada. Mathalani, kupitia Kamati ya Haki za Wasanii iliyopo chini ya Bodi ya Filamu Tanzania, zilibainika kesi kadhaa za waandishi kuibiwa, kunakiliwa na

kutumiwa kazi zao bila idhini na malipo sahihi. Hali hii imesababisha waandishi kutopata faida stahiki kutokana na kazi zao za kibunifu. Hatimaye, huchangia kuporomoka kwa ubora wa miswada.

**Mapendekezo ya Kupunguza Changamoto za Uandishi wa Miswada ya Filamu Kiswahili**

Kutokana na changamoto zilizobainishwa, inapendekezwa kutengenezwa kwa mitaala mifupi ya kimkakati wa kufundisha watayarishaji wa filamu walio katika fani. Hii ni kwa imani kuwa mafunzo haya yatasaidia katika kuboresha uandishi wa miswada kwa waandishi. Zaidi, yatanyanyua mchakato mzima wa uyatarishaji wa filamu nchini Tanzania. Katika mafunzo haya, waandishi waelekezwe kufanya uchunguzi wa kina kabla ya kuyaweka mawazo yao katika mswada wa filamu. Vilevile, inapendekezwa itengenezwe programu maalumu ya uatamizi kwa waandishi wa miswada ya filamu. Mafunzo atamizi yafanyike kwa kuwakusanya waandishi chipukizi wa miswada ya filamu na kuwapatia mbinu anuai za uandishi wa miswada ya filamu. Programu ya namna hii itazalisha waandishi wengi watakaoweza kubeba falsafa, utamaduni na idili za kifani katika maandiko yao yatakayojenga filamu bora za Kitanzania.

Aidha, ili kuinua ushindani wa kuandika miswada bora ya filamu za Kiswahili, inapendekezwa kuanzishwa kwa mashindano ya uandishi wa miswada ya filamu kwa nchi nzima. Katika mashindano haya, miswada bora mitano itachukuliwa na kutengeneza filamu za mfano ambazo zitaamsha ari na motisha ya kunyanyua tasnia ya filamu za Kiswahili za Tanzania. Vilevile, inapendekezwa vyuo vikuu kupitia idara zinazotoa kozi za Lugha ya Kiswahili na Fasihi yake, vianzishe masomo au/na kozi

maalumu zitazolenga uandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili. Zaidi, viwe na masomo yatakayohusu mbinu za ubadilishaji wa kazi mfano za Fasihi ya Kiswahili kwenda katika filamu.

Vilevile, inapendekezwa kuwa vyuo vya kati, kama vile Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), vianzishe kozi zitakazotoa masomo yanayohusisha utengenezaji na utayarishaji wa filamu. Kwa kufanya hivyo, vyuo hivyo vitaongeza maarifa kwa watayarishaji wa filamu wasio na vigezo vya kupata masomo katika taasisi rasmi zinazochukua ufaulu wa juu. Halikadhalika, Bodi ya Filamu Tanzania, kwa kushirikiana na taasisi nyingine za serikali, itengeneze mazingira rahisi ya upatikanaji wa taarifa na nyaraka muhimu kwa urahisi. Hili liwe likifanywa pindi waandishi wanapofanya tafiti za kuandikwa miswada ya kimkakati yenye kujenga taswira ya nchi au/na filamu zitakazobeba wasifu wa viongozi pamoja na tunu nyingine zipatikanazo nchini Tanzania. Kufanyika kwa jambo hili kutachochea ari ya waandishi wa miswada nchini Tanzania. Pia, kutapanua uhuru wa mwandishi katika kutoa mawazo yake.

## Hitimisho

Makala hii imejadili changamoto za uandishi wa miswada ya filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Kufanyika kwa utafiti uliozaa makala kulichangiwa na mitazamo na maoni ya hadhira ya filamu za Kitanzania iliyobainisha kutokuvutiwa na maudhui na fani yanayojenga filamu hizo kutokana na kutozingatia tajriba, maadili, na utamaduni wa Kitanzania. Halikadhalika, kulichangiwa na filamu hizi kutokuwa na uwezo wa kumudu ushindani wa filamu kimataifa. Ilibainika kuwa kiini kikubwa kinachochora mwonekano wa filamu ni miswada yake ambayo uandishi wake unakabiliwa na changamoto. Makala imejadili changamoto zifuatazo:

ukosefu wa elimu ya uandishi wa miswada, ufinyu wa bajeti za kutayarishia filamu za kiswahili, kutofanyika kwa utafiti kabla ya uandishi wa miswada, na upungufu wa ubunifu. Nyingine ni mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano, ukosefu wa uhuru wa ubunifu, ufinyu wa masoko, pamoja na kuzozingatiwa kwa hakimiliki. Ili kutatua changamoto hizo, makala imependekeza yafuatayo: iandikwe mitaala mifupi yenye mkakati wa kuwanoa wanatasnia ambao tayari wako katika tasnia; yaaanzishwe mashindano maalumu ya uandishi wa miswada; na zitengenezwe programu atamizi kwa waandishi wa filamu. Mapendekezo mengine ni: vyuo vya kati vianzishe kozi za utengenezaji wa filamu; idara za lugha na fasihi za vyuo vikuu ziwe na kozi mahususi zitakazogusa uandishi wa filamu; na utaratibu wa upatikanaji wa nyaraka urahisishwe, hususani inapotengenezwa filamu za kimkakati za wasifu wa viongozi pamoja na tunu nyingine adhimu za nchi ya Tanzania.

**Marejeleo**

Abdallah, S.A. (2018). *Nafasi ya Fasihi ya Watoto ya Kidijiti katika Kukuza Fasihi Simulizi: Mifano kutoka Vibonzo Jongevu* (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Abel, R. (1994). *The Cine Goes Town: French Cinema 1896 - 1914*. Berkeley: University of Carlifornia Press.

Giannetti, L.B. (1986). *Flashback: A brief History of Film*. New Jersey: Prentice Hall. Print.

Gumbo, M. (2019). *Practices Involved in The Design and Use of Costumes in Bongo Movies*, PhD Thesis (unpublished). Dodoma: University of Dodoma, Dodoma.

Howard, D. na Mabley, E (1993). *The Tools of Screenwriting: A Writer's Guide to the Element of Craft and Screenplay*. New York: St. Martin's Griffin.

Kabyemela, J. (2017). *The Contribution of Tanzanian Film Industry Towards Youth Employment in Tanzania*: *A case of Selected Film Companies* (Ph.D. Thesis, unpublished). University of Dodoma, Dodoma.

Kasiga, G.A. (2024). Sababu za Kutumiwa U-Nigeria katika Filamu za Kiswahili Nchini Tanzania. *Dira ya Lugha*, 1 (1), 165-175.

Kasiga, G.A. (2022). *Tathimini ya U-Nigeria katika Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya wa Kiswahili Nchini Tanzania* (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Kasiga, G.A. na Luhwago, N. (2020). Filamu ya Kiswahili: Fasihi Simulizi Iliyostawi. *Mwanga wa Lugha*, 5 (1), 107-124.

Kasiga, G.A. (2018). U-Nigeria: Athari zake katika Filamu za Kiswahili nchini Tanzania. *Mulika*, 37, 72-84.

Kasiga, G. (2013). *U-Nigeria katika Filamu za Ki-Tanzania: Chanzo, Sababu za Kutumiwa na Athari zake kwa Wa-Tanzania* (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Mahenge, E. (2016). *Drama za Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Majembe, O.M. (2023). *Cinematographic Practices and Their Effectiveness to the Quality of the Selected Tanzanian Films* (Tasnifu ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

McKee, R (1997). *Story: Substance, Structure, Style and the Principles of Screenwriting*. New York: New ReganBooks.

Mrikaria, S. E. (2007). Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya. *Swahili Forum* (14), 197-206.

Newman, L. (2007). *Social Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches*. India: Dorling Kindersley.

Shukla, P. (2013). Film as a Narrative Fiction. *European Academic Research*, 1 (9), 2722-2735.

Wafula, R. M., na Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.